Bei za mizinga ya kisasa ni za juu kuliko ile ya asili. Hata hivyo, faida zitikanazo na matumizi yake ni kubwa kuliko zile za mizinga ya asili, licha ya bei zake kuwa kubwa. Mzinga unaopendekezwa kwa mfugaji mwenye mtaji mdogo ni mzinga wa miche wa mpito wa Tanzania kwa sababu ni rahisi kwa bei na matumizi kuliko ule wa vihunzi wa biashara wa Tanzania

Mavazi ya kujikinga na nyuki
Ufugaji bora wa nyuki unahitaji kuvaa mavazi maalumu kwaajili ya kumfanya mfugaji kuwa mtulivu na salama wakati wa kuwa kabili nyuki na kwa kuepuka kung'atwa na nyuki. Mavazi hayo yanajumuisha; Ovaroli kwa ajili ya kuukinga mwili; Utaji wa uso kwa ajili ya kukinga uso; Glavu kwa ajili ya mikono; Kofia kwa ajili ya kichwa na buti kwa ajili ya kukinga miguu

Vifaa vya kuvuna mazao ya nyuki
Vifaa vifuatavyo vinahitajika kwenye ukaguzi wa mizinga na uvunaji wa mazao ya nyuki:
1. Bomba la moshi la kuwavukiza nyuki ili kuwapumbaza na kukata mawasiliano kati yao ili wasiwe wakali
2. Patasi ya mzinga ya kutenganisha mfuniko wa mzinga na viunzi au miche kwa sababu huwa vinashinikizwa na gundi ya nyuki
3. Brashi ya kuwapangusa nyuki kutoka kwenye masega kabla ya kuyahifadhi kwenye chombo cha asali
4 Ndoo safi yenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhi asali.



Kuchagua eneo la kufugia nyuki

1. Chunguza kama kuna mimea ya kutosha ya maua
2. Chunguza kama kuna maji ya kutosha. Endapo hakuna maji, wawekeemaji kwa kuchimba kisima
3. Eneo lisiwe na mafuriko ya mara kwa mara ili mizinga yako isizolewe na maji
4. Eneo liwe linapitika nyakati zote za mwaka na liwe na kivuli cha kutosha
5. Eneo lisiwe na maadui wa mizinga na nyuki kwa mfano nondo, nyegere,wezi, mchwa n.k.
6. Eneo liwe mbali na shughuli za jumuiya mfano, makazi ya watu, soko, kanisa, shule, msikiti, hospitali n.k. ili kupunguza bughudha kwa wahusika

Kutega makundi ya nyuki ili kuanza ufugaji

1. Mizinga mipya kabla ya kutundikwa huwekwa chambo. Nta iliyoyeyushwa hupakazwa ndani ya mzinga ambapo hutoa harufu ambayo huwavutia nyuki
2. Njia nyingine ni kugawanya kundi kubwa la nyuki na kugawia kwenye mzinga mpya. Masega mawili, moja lenye majana na mayai na moja lenye asali au chavua na nyuki wasiopungua 100 huhamishiwa kwenye mzinga mpya. Mzinga mpya unawekwa pale ambapo mzinga wa zamani ulipokuwa na wa zamani unahamishwa
3. Njia nyingine ni kukamata makundi ya nyuki yaliyijikusanya kwenye tawi la mti na kulikung'utia ndani ya mzinga mpya

Kimetolewa na
Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii,
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
S. L. P 3009, Chuo Kikuu,
MOROGORO TANZANIA
Tel. Gen. Line 255 023 2603511/4 Ext. 4601
E-mail: forestry@suanet.ac.tz

Sokoine University of Agriculture

College of Forestry,Wildlife and Tourism

# UFUGAJI BORA WA NYUKI



## Ufugaji wa nyuki ni nini?
Ufugaji nyuki ni kuhifadhi nyuki (wanaouma na wasiouma) ndani ya mizinga kwa madhumuni ya kupata mazao ya nyuki kama vile asali, nta, gundi n.k.

## Nyuki hufugwa wapi?
Nyuki wanaweza kufugwa mahali popote penye mimea (uoto wa asili na mashambani) inayotoa maua ya kutosha.

## Umuhimu na faida za kufuga nyuki
1. Tunapata asali, nta, gundi ya nyuki na mazao mengine. Asali n anta ni bidhaa zenye thamani kwa maisha ya binadamu
2. Mauzo ya asali n anta huongeza pato la kaya na mtu binafsi
3. Mazao ya nyuki husaidia watu kuanzisha watu kuanzisha biashara ndogo ndogo kama za pombe ya asali, kutengeneza na kuuza mishumaa, dawa ya ngozi na dawa za kuchua kutokana na nta.
4. Nyuki husaidia kuchavusha mimea ya aina mbali mbali na kwa kufanya hivyo huongeza mazao ya kilimo na yaliyo bora.
5. Ufugaji nyuki hauhitaji ardhi iliyo nzuri kama ilivyo kwa kilimo au mifugo.
6. Ufugaji nyuki hauhitaji mtaji mkubwa.
7. Vifaa vya kutengenezea mizinga hupatikana popote na kwa urahisi.
8. Nyuki wanakusanya chavua na mbochi kutoka kwenye maua vitu ambavyo ni asilia, hivyo hawahitaji chakula kingine cha ziada kama wanyama wafugwao
9. Nyuki hawahitaji uangalifu wa kila siku kama wanyama wengine wafugwao
10. Ufugaji wa nyuki waweza kufanywa na wanaume na wanawake wa rika zote
11. Ufugaji wa nyuki unasaidia mtu kujianzishia shighuli za kujitegemea
12. Ufugaji nyuki huanzisha biashara nyingine kwa wadau mbali mbali kama vile mafundi seremala wanaotengeneza mizinga, mafundi wa mabomba ya moshi, patasi za mzinga n.k.

## Matabaka ya nyuki
Kwenye kundi moja la nyuki kuna aina(tabaka) tatu kama ifuatavyo:




## Malkia (Queen)

1. Kundi la nyuki huwa na malkia mmoja tu
2. Viungo vyake vya uzazi ni kamilifu hivyo kazi yake ni kutaga mayai
3. Kazi nyingine za malkia ni kuongoza shughuli zote za kundi na kudhibiti kukua kwa viungo vya uzazi vya nyuki vibarua kwa kutumia kemikali maalum (feromoni)

## Dume (Drone)

1. Viungo vya dume ni kamilifu kama ilivyo kwa malkia
2. Nyuki dume ana jukumu moja kuu, ambalo ni kujamiiana na malkia
3. Wakati wa joto kali husaidia kupooza mzinga kwa kupepea na mbawa zake
4. Kundi moja la nyuki huwa na idadi ya madume wapatao 2,000 au pungufu kidogo

## Kibarua (Worker)
1. Nyuki kibarua kama alivyo malkia ni wa jinsia ya kike
2. Viungo vyake vya uzazi siyo kamilifu, kwa hiyo ni tasa
3. Mwiba wake una ncha kali na umezungukwa na viopoo kwa ajili ya kumwadhibu adui
4. Nyuki kibarua kama jina lake linavyoashiria hufanya kazi nyingi na za aina mbali mbali kwenye mzinga, kwa mfano kukusanya mbochi za chavua kwa manufaa ya wote
5. Idadi ya nuki vibarua kwenye kundi huweza kufikia 80,000

## Vifaa muhimu katika ufugaji nyuki

1. Mizinga ya kisasa
2. Mavazi ya kujikinga wakati wa kuvuna asali
3. Bomba la moshi
4. Patasi ya mzinga
5. Vifaa vya kukamulia asali
6. Vifaa vya kutengenezea nta
7. Vifaa vya kuhifadhi asali na nta

## Mizinga
Mizinga ni 'nyumba' ya makundi ya nyuki. Mizinga inayotumika Tanzania imegawanyika kwenye makundi mawili makuu: Mizinga ya asili na mizinga ya kisasa

## Matatizo ya kutumia mizinga ya asili
1. Ukaguzi ni mgumu, kwa vile masega yake hayawezi kusogezwa
2. Uvunaji ni wa kuondoa masega yote, hivyo kuharibu masega ya majana na kuwaua nyuki wengi
3. Mizinga hii haidumu kwa vile huoza au kuharibika mapema kutokana na mali ghafi iliyotengenezewa
4. Uharibifu wa mazingira kwa kutumia mizinga ya magome ya miti. Miti iliyobanduliwa hukauka
5. Kupunguza vianzo vya maua. Miti mingi inayofaa kwa mizinga ya asili ni miti itoayo maua ambayo ni vyanzo muhimu vya mbochi na chavua, ambavyo ni chakula cha nyuki na binadamu.

## Mizinga ya kisasa

Hii ni mizinga iliyobuniwa na kutengenezwa mithili ya sanduku la mbao kwa vipimo na utaalamu maalumu. Mizinga ya kisasa inayotumika hapa Tanzania ni ya aina mbili:

1. Mzinga wa mche, mfano Mzinga wa Mpito wa Tanzania



2. Mzinga wa viunzi, mfano Mzinga wa Biashara wa Tanzania



## Faida za kutumia mizinga ya kisasa

1. Urahisi wa kusogeza masega, kwa kusogeza miche au viunzi wakati wa ukaguzi wa makundi ya nyuki na wakati wa uvunaji
2. Mavuno ya asali ni mengi na bora
3. Kwenye mizinga hii nirahisi kuvuna masega yenye asali na kuyaacha yenye majana na matupu
4. Matumizi bora ya mbao na kupunguza uharibifu wa mazingira.